JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA

Barabara ya Nyerere
S.L.P 377 Musoma
Simu: 028-2623029 Nukushi :028- 2623030
Barua pepe: rbcmara@pccb.go.tz
Wavuti www.pccb.go.tz

TAARIFA KWA UMMA

MARA JULAI 21, 2020

TAKUKURU MKOA WA MARA YAOKOA TSH 1.0 96 BILIONI

Ndugu wana Habari,

Kwa takriban ndani ya mwezi mmoja TAKUKURU Mkoa wa MARA imekuwa ikifanya uchunguzi kuhusiana na ufisadi katika malipo ya fidia katika kijiji cha MATONGO Wilayani TARIME. Katika uchunguzi huu TAKUKURU imeweza kubaini mambo makubwa yafuatayo:-

Kwanza, suala la 'tegesha' katika Wilaya ya Tarime limekuwa ni donda ndugu lililokosa wa kulikemea kwa ujasiri. Suala la tegesha linao utetezi wa kisiasa na ndiyo maana hakuna mwana siasa hata mmoja kutoka chama chochote kile aliyewahi kusimama na kukemea uchafu na aibu hii ya kutegesha.

Tunapozungumzia TEGESHA tunamaanisha ni utaratibu au makubaliano yanayofanyika kati ya Wathamini (Valuers) na wananchi wakazi wa eneo fulani pale wanapotakiwa kupata taarifa ya tathimini ya mali walizonazo kwa ajili ya kuandaliwa malipo fulani.

Pili, watumishi wa Serikali ambao kimsingi tulitegemea wawe mstari wa mbele kukemea tabia hiyo ndiyo walikuwa mstari wa mbele kuukingia kifua ufisadi huo na hata wengine kuwa miongoni mwa wadai katika madai hayo.

Tatu, zoezi zima la tegesha lilibebwa na watu wenye nguvu za kifedha na kiwadhifa kiasi cha kutofanywa chochote kwa muda wote ambao zoezi la tegesha limekuwa likiendelea.

Kifupi tegesha ni zoezi chafu linalolitia **Taifa aibu kwani linawaumiza pia wawekezaji kutoka nje.** Ni zoezi linalothibitisha kukosa uzalendo kwa wathamini wake (Valuers) na ni aibu kwa taaluma ya wathamini kitu kilichokwisha kuhalalishwa na hakuna aliyewahi kuingilia kati.

Ndugu wana Habari,

Uchunguzi huu ulikumbana na nguvu kali za kisiasa na kijamii kwa madai kuwa tegesha ndiyo uchumi kwa wana - nyamongo na kwa hiyo kujaribu kuingilia kati zoezi hili maana yake ni kuangusha uchumi wa wana - nyamongo. Kifupi uchunguzi ulikuwa mgumu sana.

Katika uchunguzi huu sehemu ya pili TAKUKURU ilishughulika na jumla ya chunguzi 28 zilizobainika kuwa na thamini zenye thamani ya sh **2,056,451,700/=** zilifanyiwa kazi.

- Katika thamini hizi 28 chunguzi 15 zenye thamini 15 zenye thamani ya sh 1,119,550,915 zimekamilika.

- Katika uchuguzi huu TAKUKURU tulibaini kuwa kiasi cha fedha kilichotakiwa kulipwa kwa thamini hizo 15 ni **sh 64,000,000/=** tu lakini fedha zilizolipwa ni 1,119,550,915/ na hivyo kumaanisha kuwa kiasi cha **Sh. 1,055,550,915/-** sawa na **1,649.3% kuwa ni zao la ufisadi.**

Ndugu wana Habari,

Kazi tuliyoifanya kubwa katika hatua za awali ni kuhakikisha fedha hizi zinarejeshwa kutoka mikono michafu na tumefanikiwa kwa kipindi cha mwezi mmoja kurejesha kiasi hicho cha **sh 1,055,550,915/-** (Bilioni moja na milioni hamsini na tano, laki tano na hamsini elfu mia tisa kumi na tano)

Mbali na wananchi hao 15, wapo wananchi wengine 13 ambao thamini zao zinaonekana kuwa walistahili kulipwa kiasi cha **sh 31,444,346** badala yake walilipwa kiasi cha **sh 936,900,785/=.**

Watuhumiwa hawa wamekimbia mji na hawajulikani waliko. Wananchi hao ambao akaunti zao tumezizuia kwa muda walilipwa malipo hewa ya kiasi cha **sh 905,456,348/** kiasi ambacho ni sawa na **2,879.6%** ya malipo waliyostahili kulipwa.

TAKUKURU Mkoa wa Mara tunaendelea kuwatafuta watuhumiwa hawa ili warejeshe fedha hizo na fedha zao zipo benki.

Vilevile, Uchunguzi wa TAKUKURU umebaini kuwa kiasi ambacho kilitakiwa kulipwa kupitia thamini hizi 13 ni kiasi cha **sh. 31,444,346/=** na hivyo kufanya malipo ya kiasi cha **sh. 905,456,438/=** kuwa ni hewa. Ufisadi huu ni sawa na **2,879.6%**

Kwa hawa waliokimbia naomba kutumia nafasi hii kuwataka wajisalimishe katika ofisi za TAKUKURU Mkoa wa MARA kwa mazungumzo ya kurejesha fedha walizopokea kwa makosa vinginevyo hawatabaki salama.

Ndugu wana Habari,

Zaidi ya kuokoa fedha hizi, TAKUKURU imeendelea pia na zoezi ililolianzisha kuwasaidia wastaafu ambapo kwa mara nyingine tumeweza kuokoa kiasi cha sh 41,300,000/= na hivyo kufanya jumla ya fedha ambazo tumeokoa mpaka sasa (taslimu) kuwa **sh 1,096,850,915/** kwa kipindi hiki kifupi.

Tunashukuru kwa kupewa heshima ya kusimamia uchunguzi huu ambao ni wa kwanza na wa aina yake. Kutokana na madudu tuliyoyaibua Nyamongo, tayari TAKUKURU tumepewa kazi nyingine ya kupitia uthamini wa upanuzi wa uwanja wa ndege Musoma ambapo tayari tumeshaanza kunusa harufu ya rushwa. Chunguzi zote hizi mbili tutaziendesha kwa pamoja.

Ndugu wana Habari,

Mwisho, TAKUKURU imepokea taarifa kwamba wapo viongozi wa juu kabisa Mkoani ambao katika kipindi hiki cha uchaguzi wamekuwa wakipita kwa wanachama wa CCM na wafanyabiashara kukusanya fedha kwa madai ya kutumwa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Tanzania Mhe. DKT. JOHN POMBE JOSEPH MAGUFULI.

Hadi sasa TAKUKURU imeshakusanya ushahidi wa sh 600,000,000/= ambazo hatuamini kama Mheshimiwa RAIS anaweza kuomba fedha kupitia njia hii. Uchunguzi unaendelea na punde tutakapoukamilisha tutawasilisha taarifa.

Tunavishukuru vyombo vyote vya usalama pamoja na Taasisi zote zilizotupa ushirikiano wakati wa zoezi hili. Kuhusiana na zoezi la kupitisha wagombea, ofisi yangu inaendelea kufuatilia vitendo vichafu vya baadhi ya wagombea kushiriki moja kwa moja katika kutoa rushwa.

ALEX KUHANDA
MKUU WA TAKUKURU (M)
MARA.